

Wapendwa marafiki,

Shukurani nyingi kwa wale walioshirikiana nasi kwa kile kilichotokea siku ya tarehe 17 mwezi wa 10 katika maeneo yao.

Bi Teddy Mkami, kutoka Shinyanga, alituandikia: "Siku ya tarehe 17 mwezi wa 10 wao waliadhimisha siku hii kwa kuwatembelea watoto waishio katika mazingira magumu, hasa wale wenye mzazi mmoja au yatima kabisa."

Asante vilevile kwa wale waliowaalika marafiki zao, wafanyakazi wenzao au familia zao kusaini Mwito kwa Vitendo. Msaada wenu ulikuwa na thamani sana!

Dear friends,

Many thanks to those who shared with us what happened on October 17th in their area.

Mrs Teddy Mkami, from Shinyanga, wrote: "On the 17th, we visited children who have a more difficult life, either because they have a single parent or because they are orphans."

Thanks also to those who invited their friends, colleagues or family members to sign the Call to Action. Your support was very precious!

Jijini Dar es Salaam

Katika kusherehekea Siku ya Kimataifa ya kuutokomezwa umaskini, tuliungana na TANGO (Muungano wa NGO's za Tanzania), pamoja na vyama vingine mbalimbali, tulisaidiana kuandaa mkutano mkubwa ambao ulifanyikia Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. Wawakilishi wa ATD Fourth World walikuja kutoka Boko, Tegeta, Soko la Samaki Fery na M'nyamala, simama, sema usikike na uchukue hatua dhidi ya umaskini. Kwa niaba ya kundi Sadiki aliusoma mkusanyiko wa shuhuda. Mama Yusufu binafsi alizungumza kuhusu umuhimu wa elimu.

In Dar es Salaam

To celebrate the International Day for the Eradication of Poverty, we joined TANGO (Tanzanian Association for NGOs) and, together with other associations, we helped organizing a big meeting that took place on Mnazi Mmoja. ATD Fourth World delegations coming from Boko, Tegeta, the Fish Market and Mwananyamala stood up and spoke out. On behalf of the group, Sadiki read a collective testimony. Mama Yusufu personally spoke about the importance of education.




ATD Fourth World Movement
P.O. Box 61786
Dar es Salaam
mail : atd.tanzania@gmail.com
tel : 022 - 276 17 17



Jijini Paris

Eugen Brand (Mwakilishi mkuu wa Ushirikiano wa Kimataifa wa ATD Dunia ya Nne) alitukumbusha sisi kwamba, miaka ishiri 20 iliyopita, kwa mara ya kwanza mwito kwa vitendo ulichongwa kwenye jiwe la kumbukumbu na *"historia ya walio maskini sana iliandikwa katika historia ya ubinadamu"*.



Akirejea kampeni ya mwito kwa vitendo, Eugen alisema: *"Iwapo tunaunganisha sauti zetu, iwapo sisi (maskini na wasio-maskini) tutakaa chini pamoja tukiizunguka meza,(...) akili mpya itaibuka."*

Amani itakuwepo. Hadhi itarudi mahali pake badala ya fedheha. Kujifunza kutoka mmoja hadi mwengine kutaondoa nafasi ya ujinga na kujituma kutaleta matumaini pale palipokuwa na kukata tamaa."

Aliongeza kusema kwamba uzoefu wa watu maskini kupita kiasi vilevile ni thamani mbele ya changamoto kubwa ya dunia: mabadiliko ya hali ya hewa, utandawazi wa uchumi, mapigano, nk.

Ally na Issa walituwakilishi sisi

Walipeleka bango linaloelezea kwa mifano maisha ya watu wa machimbo ya mawe na wale wa Soko la Samaki Feri. Ujumbe wa ili bango ulikuwa: "Kazi ngumu, maisha magumu lakini matumaini sawa kwa baadae!"

In Paris

Eugen Brand (General Delegate of the International Movement ATD Fourth World) reminded us that, 20 years ago, the first call to action was engraved on the commemorative stone and *"the history of the very poor was inscribed in the history of humanity"*.

Referring to the Call to Action campaign, Eugen said: *"If we unite our voices, if we (poor and non-poor) sit down together around the table, (...) a new intelligence will emerge."*

Peace will become possible. Dignity will replace humiliation. Learning from one another will take the place of ignorance and personal commitment will give hope where once there was despair."

He added that the experience of the poorest is also precious in front of the biggest challenges of the world: climate change, globalized economy, conflicts, etc.

Ally and Issa represented us

They brought a banner illustrating the life of the people at the quarry and fish market. The message of this banner was: "Hard work, hard life, but same hope for the future!"

Walikuwa na ujumbe kutoka kwa watoto wanaowafahamu katika Dar es Salaam. Watoto hawa walishirikiana na ndoto zao na kinachowafanya wao wawe na furaha pamoja na ugumu wa maisha na familia zao.

Wakiwa Ufaransa, Ally na Issa walikutana na wawakilishi wengine, kutoka Afrika ya Kati, Madagascar, Haiti, New York nk. Kutokomeza umaskini ndicho kilichowahusisha na walizungumza kuhusu tofauti zao za kujiwekea sharti kwao. Ally na Issa wamerudi na sentensi hii ya Padri Joseph mioyoni mwao: "Kuishi katika umaskini sio aibu, umaskini ni aibu!"



They had messages of children they know in Dar es Salaam. These children shared their dreams and what makes them happy despite of the hardships of their families. Their messages joined thousands of other children's messages from around the world.

While in France, Issa and Ally met with delegations from Central Africa, Madagascar, Haiti, New York, etc. The eradication of poverty was their common concern and they spoke about their different commitments. They came back with one of Father Joseph's sayings in their heart: "To live in poverty is not a shame, poverty is a shame!"

Jijini London

Moraene Roberts ni mwanamke wa Kiingereza ambaye ni mwanachama wa muda mrefu sana wa ATD Dunia ya Nne, alikutana na Dr Asha Migiro Katibu Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa kwa muda wa dakika 15. Moraene alizungumza nae kuhusu mada za umaskini katika UK. Moraene alimwambia Dr Migiro kuhusu timu ya ATD inayofanyakazi Tanzania, na alimpatia nakala ya ripoti ya Benki ya Dunia ambamo ndani yake kuna sura inayoelezea kazi ya ATD katika Tanzania.

In London

Moraene Roberts, a British woman, member of ATD Fourth World, met with Dr Asha Rose Migiro, UN Deputy Secretary General. For about 15 mins, Moraene spoke with her about poverty issues in the UK. She told her about the team's work in Tanzania and gave her a copy of a World Bank report which contains a chapter on the ATD work in Tanzania.



Jijini New York

Wawakilishi kutoka Haiti, Philippines, France na UK walikutana na Ban Ki-Moon, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, na walimkabidhi matokeo ya kampeni ya wito kwa vitendo, saina zilizosainiwa na watu zaidi ya 150,000 kutoka nchi 160 tofauti duniani kote. Zaidi ya 400 katika Tanzania!

Ban Ki-Moon alitangaza: *“Dunia lazima itazame tena na kuelekeza rasilimali zake mahali na kwa watu ambao wameachwa nyuma.”*

In New York

A delegation of people coming from Haiti, Philippines, France, and UK met Mr Ban Ki-Moon, the UN Secretary-General. They handed him over the results of the Call to Action campaign: more than 150,000 signatures from 160 countries throughout the world. 400 from Tanzania!

Ban Ki-Moon declared: *“The world must refocus its attention and its resources on the places and people that are being left behind.”*



Tafadhali tujulisheni na pia toeni mawazo yenu na hisia zenu kuhusiana na barua hii.

Tungependa tukuulize swali moja: Je unaamini katika kuutokomeza umaskini? Kama unaamini, je ni jinsi gani umeshalifanyia kazi katika maisha yako ya kila siku?

Tunatazamia kusikia toka kwenu, tunawatakia furaha sana ya mwaka mpya!

Timu ya ATD Dunia ya Nne, Dar es Salaam

Please, let us know about your comments and reactions concerning this letter.

One question we would like to ask you is: Do you really believe in the eradication of poverty? If you do, how do you already work on it in your daily life?

Looking forward to hearing from you, we wish you a very Happy New Year!

The ATD Fourth World team in Dar es Salaam



ATD Fourth World Movement
P.O. Box 61786
Dar es Salaam
mail : atd.tanzania@gmail.com
tel : 022 - 276 17 17